# TECHNICAL UNIVERSITY OF MOMBASA

SCHOOL OF HUMANITIES AND SOCIAL SCIENCES

DEPARTMENT OF COMMUNICATION STUDIES

**UNIVERSITY EXAMINATION FOR:**

BACHELOR OF JOURNALISM & MASS COMMUNICATION

BMC 4303: AUDIO PRODUCTION

END OF SEMESTER EXAMINATION

PROJECT

**SERIES:JUNE**APRIL2017

**TIME:**Choose hoursPROJECT

**DATE:**Pick DateSep2017

**Instructions to Candidates**

You should have the following to be graded for this examination

*Final recording on CD. Each candidate must present an examination pass and student ID when submitting the final project.*

This is a project; you are therefore expected to attempt all questionsChoose No. AttemptALL questions

---

Project (group project) 70 marks

Using the attached script, cast and record a radio drama with all the necessary sound effects and to make the final project as convincing as possible.

PROGRAM TITTLE: KIKULACHO KI NGUONI MWAKO

FORMAT : DRAMA

LANGUAGE : SWAHILI

DURATION : 15 min

TARGET : COASTAL COMMUNITIES

STATION : TBA

PRODUCER : GALGALO BOCHA

**CONTROLS: PLAY SIGNATURE TUNE FOR 15" THEN FADE OUT UNDER**

**ANNOUNCER**: Hujambo msikilizaji na karibu katika mchezo wa kikulacho ki nguoni mwako. Huu ni mchezo wa redio unaoangazia matatizo ya madawa ya kulevya na jinsi mwanajuma, mama mmoja katika kijiji cha mrani alivoamua kupigana na uuzaji ma mihadarati mtaani. Azma ya mwanajuma ilichochewa baada ya mwanaye wa kwanza saidi aliyekuwa mraibu wa madawa ya kulevya kuuawa na umati wa watu alipokuwa akijaribu kumwibia mama mmoja katika eneo la mwembe tayari. Majina yaliyotumiwa katika mchezo huu ni ya kubuni wala hayahusiani kamwe na familia yoyote.

**CONTROLS SNEAK THEME MUSIC THEN CROSS FADE WITH FX**

**FX: VILLAGERS SHOUTING**

MVO 1 : Leo utatutambua, kila siku mwaibia watu hapa (FX slap)

MVO 2 : Hakuna judadiliana na mwizi muuaji, jangili, tena teja mraibu wa madawa ya kulevya

Voices : Ua maliza, Maliza mwinzi,……….

FVO : Yaani kila siku hatuwezi kutembea kwa sababu yenu

MVO 3 : Tafadhali msininue mimi nilikuwa…..najaribu tu kujipatia riziki.

MVO 1 : kuibia watu ndio kujopatia riziki …..leo utakufa wewe ….hebu nileteeni tairi. Majangili kama hawa ni kuua tu.

FVO : Huyu si ni mtoto wa mwanajuma……uui tafadhali msimuue

MVO 2 : Mama toka hapa tuachie

Voices : Teketeza kabisa, uaa

**CONTROLS:SNEAK BRIDGE MUSIC, HOLD FOR 10" THEN FADE OUT**

## ONYESHO LA PILI

**FX: FOOTSTEPS RUNNING AND HEAVY BREATHING.**

Kibibi : (azungumza huku akiwa anahema kwa nguvu)..bi mwanajuma njoo haraka…..wanamuua mwanao……eti jambazi…

Mwanajuma : (Alia kwa huzuni)..mwanangu eti jambazi…..nani hao, mwanangu yupi…

Kibibi : eti ni mraibu mwizi na….

Mwanajuma : wapi

Kibibi : Pale mwembe tayari kwa chifu

Mwanajuma : Yaani ijumaa mchana mwanangu auawe kwa chifu…..chifu mwenyewe ndiye aliwaamuru? Najua huwa hampendi huyo motto wangu jamani mimi nitaenda wapi……mungu nilikosea wapi? Aah

Kibibi : Pole mama, uzito wa ulezi ni wetu kinamama

Mwanajuma : jamani wanangu wote waangamia kutokana na madawa ya kulevya (sobs) …...lakini nitafanya kila niwezalo……..nisikike ama niangamie na wanangu….

**CONTROLS: SNEAK BRIDGE HOLD 10" THEN FADE OUT**

## ONYESHO LA TATU

**CONTROLS: PLAY SOFT INSTUMENTAL**

Mwanajuma : (Soliloquies) Nimemzika mwanangu saidi, aliyeuawa kwa kujihusisha na uhuni ili kujipatia pesa za kununua mihadarati……eeeh sasa tena naambiwa mwanangu wa pili kaambukizwa hepatitis B……..mhhh yote ni kutokana na mihadarati. Je tutailaumu serikali….nimlaumu mungu….au ni mimi ndiye nilikosa kutimiza wajibu wangu kama mzazi?.....lakini anayeuza mihadarati hii si ni ndugu yangu jando, ndugu tumbo moja kanimalizia wanangu? (Sobs)

FX : Knock on the door

Mwanajuma : Karibu ndani….

FX : Door opens and closes gently

Mwanajuma: (surprised)….jandoo ni wewe, (kwa hasira) umekuja nini hapa kwangu…shetani wewe…

Jando : (kwa upole) Dadangu nimekuja kukupa pole

Mwanajuma : (interjects) Pole! ……Pole kweli au ni kuja kuona madhara uliyo niletea..

Jando : Madhara gani tena dada (kwa upole) kwanza chukua hizi hapa hizi zitakufaa wakati huu wa msiba

Mwanajuma : (mimics) chukua hizi zikufae wakati huu wa msiba….jando hii mihadarati yoote inayowauwa watoto hapa mtaani aneyeileta ni nani…….halafu waja hapa eti kunifariji…..je wanao pia unawapa hizo tembe?

Jando ; kwangu ni bashara…

Mwanajuma : Biashara kweli…..sitaki kukuona tena hapa kwangu na sitaki msaada wowote kutoka kwako….mwanaharamu wewe…..nenda…bado wasubiri nini hapa?

Jando : Haya kwaheri lakini usirudie hayo maneno uliyoyasema inje ya nyuma hii…la sivyo…..

Mwanajuma :(amkatiza kwa hasira) La sivyo nini, utaniua vile ulivyowaua wanangu…..

Jando : Nakuonya wewe……… tusianze vita

Mwanajuma : Basi vita vimeanza………..uniuwe pamoja na wanangu……mimi sikuogopi kama wale wengine.

Jando : nakwambia hutaniweza…..

Mwanajuma : nilikwambia uondoke hapa ibilisi wewe…..

**FX : Door opens then bangs**

Mwanajuma : Shetani wewe….

**<u>CONTROLS: SNEAK BRIDGE HOLD 10” THEN CROSS FADE WITH FX</u>**

## ONYESHO LA NNE

FX: street ambience

Kibibi : Vipi mwanajuma hajuaonana tangu tuhitimishe…….habari za kwako

Mwanajuma : Niko sawa….

Kibibi : Lakini mbona uso huo wa hasira

Mwanajuma : Si nilikuambia Yule ibilisi jando alikuja kwangu na kunitisha, sasa ameanza kuwatuma watu kuniambia niwache kuwashawishi akina mama kupiga vita mihadarati mtaani kwetu.

Kibibi : (Kwa sauti ya chini) lakini hawa wauzaji mihadarati ni watu hatari….chunga mwenzangu.

Mwanajuma : Kibibi, wajua nimepoteza watoto kutokana na mihadarati, mmoja nimemzika…wa pili namuuguza kisha waniambia hatari….hatari gani?

Kibibi : Si hivyo mwenzangu usinielewe vibaya

Mwanajuma : Tukishikana sote tupige sauti, tuandamane mitaani, mijini na kuvutia vyombo vya habari…hili tatizo litaisha…..na lisipoisha litapungua.

Kibibi : sasa tufanyaje?

Mwanajuma : Mimi nimewasajili akina mama 200 tayari, jumanne ijayo tutaenda kwa kamishna wa kaunti…..hili jambo ni lazima liishe.

Kibibi : Tuko pamoja

Mwanajuma : Tumesimama sana hapa hebu nipeleke pale kwa mzee hamisi nikachukue sukari…tuondoke hapa hao mateja wa jando wasije wakatubakura mikoba.

**CONTROLS: SNEAK BRIDGE HOLD 10" THEN FADE OUT**

## ONYESHO LA TANO

**FX: PHONE RINGS**

Mwanajuma : (anajiongelesha) Simu ya nani usiku huu….Helo nani mwenzangu…halooo

VO : wachana na hiyo mipango yako la sivyo utakiona cha mtema kuni…

Mwanajuma : Mipango gani? Kama wewe ni jando ama ukiwa umetumwa naye basi mwambie cha mtema kuni nilikona pale alipowafunza wanangu kutumia mihadarati… (anajiongelesha) shenzi huyu anakatia nani simu.

**CONTROLS: SNEAK BRIDGE HOLD 10" THEN FADE OUT**

## ONYESHO LA SITA

Mwanajuma : a kina mama, leo nimewaita hapa ili tupange jinsi tutakavyo kabiliana na hili janga. Tusikubali kuwapoteza watoto wetu tena. Akina mama hoyee

VOICES : Hoyeee

Mwanajuma : Kesho tunaenda kwa kamishna, mimi nimetishiwa….nimeambiwa niachane na hii mipango…lakini ni lazima nipigane. Mimi najua uchungu wa kumpoteza mototo. Tusitishike maanake tunapigania watoto wetu

FX : Ululation

Mwanajuma : Mimi niko tayari kufa, jana waliteketeza nyumba yangu, wengine wetu wamejiondoa katika vita hivi. Lakini nawaambia tushikane tuangamize mihadarati hapa kwetu. Anayesambaza mihadarati hapa ni ndugu yangu tumbo moja…….mimi sijali lazima twende mbele.

VOICES : mihadarati marufuku tusilegeze kamba.

**CONTROLS: SNEAK BRIDGE HOLD 10" THEN FADE OUT**

## ONYESHO LA SABA

Kibibi : mwenzangu jambo tulilolifanya hapa kijijini ni kubwa mno, yaani jando ametiwa nguvuni?

Mwanajuma : lazima wengine pia watiwe nguvuni huu mtaa lazima uwe safi…tusipoteze watoto wetu ovyo.

Kibibi : Kila mwana kijiji yuakusifu

Mwanajuma : Kilichotendeka ni juhudi za wananchi, akina mama…tukishikana tutamaliza aina yoyote ya shida inayotukabili.

Kibibi :aah nilikuwa nimesahau, akina mama wamenituma nikuambie kuwa wako tayari kuchanga ili kukuwezesha kujenga tena nyumba yako iliyoteketezwa na jangili lile.

Mwanajuma : has ante saana, lakini nimearifiwa kutoka katika afisi ya kamishna kuwa ninahitajika ikulu ya rais ili kutuzwa kutokana na juhudi zetu hapa mtaani.

Kibibi : Juhudi zako hatimaye zimetambuliwa

Mwanajuma : Ni juhudi za kila mama hapa mtaani….. mini nitalilia uongozi wan chi kukaza kamba katika vita hivi.

Kibibi : Basi usisahau kulilia kujengewa nyumba nyingine.

Mwanajuma: Cha muhimu ni kuwa sauti yetu imesikika.

**CONTROLS: SNEAK BRIDGE HOLD 10" THEN FADE OUT**

Announcer: Kufikia hapo ndipo tunatamatisha mchezo wetu kikulacho ki nguoni mwako, mchezo huu umetayarishwa nami galgalo bocha. Kwa niaba ya wote walioshiriki na kuaga kwaheri.